Red Rock Canyon National Conservation Area
Genge la Jiwe Nyekundu Eneo la Hifadhi ya Taifa
Nafasi za Kuburudika

Kwenye Kituo cha Wageni kuna maonyesho ya undani na ya nje, duka la zawadi, sinema, na vyuo vyenye maji ya mabomba. Vyupa vya maji na vinywaji vya michezo vinauzwa humo.
Barabara ya mandhari nzuri ndiyo barabara ya njia moja ya kilomita 21 (maili 13) yenye maegesho ya magari na vyanzo vya njia za ketembea mbali mrefu. Njia za kutembea hizi, yale rahisi na yalio ngumu, yanaanza pale pale kwenye vyanzo vya nija za kutembea mbali mrefu (trail heads). Vyuo bila maji vinapatikana kwenye maegesho ya magari mbalimbali. **Hadharini:** Maji ya kunyunwa hayapatikani mahali po pote kwenye Barabara ya Mandhari Nzuri.
Genge la Jiwe Nyekundu ndiyo mahali maarufu sana kwa wapandaji mawe. Nafasi za kupanda mawe kwa kutumia makamba na bila makamba (bouldering) kwenye urefu mbalimbali kwa wale wenye uzoefu zote zinapatikana.
Wale wanokimiba kwa kutumia baiskeli wanaruhusiwa kwenye. **Tafadhali**: Muwe waangalifu kwa wale wanaotembea barabarani kwa baiskeli na kwa wanyama mwitu pia. Asante.
Baisheliza Milima (mountain bikes) zinaruhusiwa karibu na Almasi ya Blu na Bonde la Cottonwood.
Wakati ulio bora kwa kuwaona wanyama mwitu ndiye masaa ya asubuhi na mapema na jioni na mapema.
Wakati ulio bora kuyaona maua ya mwitu ndio wakati wa majira ya kuchipua na miezi ya chanzo cha majira ya jioto.
Kutembea kwa kutumia farasi kunaruhusiwa kwenye njia mbalimbali. Magari ya kubeba farasi yanaruhusiwa kuegesha kwenye maegesho ya magari ya Jiwe Nyeupe, Chemchemi ya Willow na Scenic Drive ili kurahisisha njia kwa wapandaji farasi kuingia njia za kutembea.
Vibali vinajitajika kwa harusi, kupigapicha za biashara, na kwa shughuli za makundi makubwa (zaidi ya watu 15). Maarifa juu ya vibali inapatikana kwenye Kituo cha Wageni.

Usalama

Ukiwaona wanyama wa mwitu, muwe waangalifu. Msiwalishe wanyama wala usigeuke upande. Wanaweza kukung'ata, kukuchoma, kukupiga teke na kukuuma. Muwe waangalifu po pote utakapoweka mikono na miguu ili kuepukana na nyoka, wadudu, buibui, nge na mjusi. Musiguse wala kuchuma mimea. Mimea mingi ina miiba inaouma na kuchoma.
Kabla hujaingia hakikishe kwamba mnayo maji ya kutosha. Mlete angalao lita moja ya maji kwa kila mtu kwenye kundi lako. Mkipanga kutembea umbali, mlete lita kadhaa kwa kila mtu.
Soma kwa hadhari maelezo ya kila njia kabla hujaanza kutembea. Msitembee mbali kwa kutumia njia iliyo ngumu kuliko uwezo wenu. Muwe waangalifu zaidi mtakapotembea wakati wa jua kali.

Sehemu Muhimu za Zamani za Kale

Ingawa ipo kwenye jangwa kavu, chemchemi na mahali penye bakuli za mawe yanayohifadhika maji yapo. Bakuli za mawe hayo yanaitwa *tinajas* kwa lugha ya asili. Maji hayo yanasaidia kutunza mimea na wanyama wa jangwa ili kudumu katika mazingira ya ukali. Makabila ya Paiutes ya Kusini na Pueblo wa Kale na makabila mengine ya Waamerica wa Asili walizoea kutuma sehemu hii kwa kukusanya maji na vyakula.

Tundu la kuchoma nyama (Roasting pit)

Roasting pits ndiyo mashimo ya mviringo mdogo yaliochomwa kwenye mawe ya chokaa lililotumiwa kwa kupikia vyakula vya mimea na nyama. Mingine ndiyo mawe ya mviringo mdogo. Mingine ilikuwa na urefu wa mita kadhaa. Matundu ya kuchoma hayo yanapatikana karibu na maegesho ya magari na njia za kutembea mbali mrefu (trailheads) ya Sandstone Quarry, White Rock na Willow Spring.

Sanaa za Mawe (Rock Art)

Kuna aina mbili za Rock Art: *Petroglyphs* na *Pictographs*.
Petroglyphs ndiyo picha zinazoparuiwa kwenye mawe yenyewe.
Pictograph ndiyo picha zinazochorwa juu ya uso wa jiwe fulani.
Sanaa za mawe za aina zote zinaonekana pale Red Spring na Willow Spring kwenye sehemu za mandhari.
Tafadhali! Musiguse sanaa za mawe yo yote. Ni ya kale mno na yanavunjika upesi.

Sehemu Muhimu Yaliyo ya Desturi za Ulaya

Njia ya Kihispania (Spanish Trail)

Kati ya miaka 1829 hadi 1830, Spanish Trail ilianzishwa na wapelelezi wa Hispania kuwa njia ya biashara kutoka kwa Santa Fe, New Mexico mpaka Los Angeles, California. Sehemu za njia hii zinapitisha Red Rock

Canyon. Mara Spanish Trail ilipoanzishwa, wapelelezi, wafanya biashara, wachimbuaji wa mawe, makundi ya dini na waloezi waliitumia kusafiri mpaka California na kurudi tena.

Barabara ya Wamormon (Mormon Road)

Kati ya miaka 1840 na 1849, watu wa dini ya Kimormon walifafirisha bidhaa kwa kutumia njia fulani iliyopitisha Red Rock Canyon. Siku hizi, njia hii inaitwa Mormon Trail. Iliunganisha Salt Lake City, Utah na jimbo la California. Ilikuwa njia iliyopendelewa kwa wale waliosafiri kwa kutumia magari yaliyovutwa na farasi ama ng'ombe.

Mashamba ya mifugo na Uchimbuaji

Kati ya miaka ya mwisho wa ya karne ya 1800 na miaka ya kwanza ya karne ya 1900, watu walifuga ng'ombe na kondoo na kulima mazao karibu na sehemu ya First Creek, Pine Creek na Calico Basin.

Uchimbuaji wa mawe mchanga ilitokea pale Sandstone Quarry. Uchimbuaji wa fedha ilitokea pale La Madre Spring. Uchimbuaji wa jasi ilitokea pale karibu na kijiji cha Blue Diamond.

Historia ya Jiolojia

Upande wa Chini ya Bahari

Kadiri ya miaka 542-251 milioni yaliyopita (Paleozoic Era), Red Rock Canyon ilikuwa upande wa chini ya Bahari. Wanyama wengi wa Bahari waliishi kwenye maji haya na walipokufa waliyabakiza makombe, simbi na viunzi vya mifupa. Mashapo yaliacha tabaka za chokaa.

Uumbaji wa nchi

Mabadiliko na mahamisho ya ardhi yalipandisha chokaa kutoka kwa chini ya bahari juu ya usawa wa bahari, na kuumba nchi kavu. Mabadaliko na mahamisho hayo yaliumba baadhi ya milima tunayoiona leo. Machanga yalikusanyika hapahapa kadiri ya miaka 180 milioni iliyopita. Chungu ya mchanga ilitokea. Mvua yalisaidia kubadilisha hiyo chungu ya mchanga zifanyike kuwa mawe ya mchanga. Chuma kwenye mchanga iliweka rangi nyekundu na ya machungwa kwenye milima hii ya mawe ya mchanga.

Keystone Thrust Fault Line

The Keystone Thrust Fault ni mvunjiko kwenye uso wa ardhi ambayo nguvu kubwa ilikunjika mawe kwenye rusu. Jambo hili lilisababisha mawe ya mchanga ya kale kuonekana juu ya mawe ya mchanga yaliyo ya juzijuzi. Hali hii si ya kawaida kwenye mawe ya mchanga.

Mmomonyoko

Uchanganyiko wa joto kali, hali ya baridi ya kiwango cha kuganda, upepo, mvua na gharika unaathiri milima. Mambo hayo yanayoitwa mmomonyoko (erosion) yanavunja na kugawanya mawe, kufanya ufa kwenye mawe, kulainisha mawe na kuendelea kubadilisha uso wa milima mpaka leo.

Aina za Mawe/Madini

Bonanza King Limestone (Milima ya mawe ya kijivu)

Bonanza King Limestone inaonekana kwenye eneo hii. Iliumbwa chini ya bahari kutoka kwa *calcium carbonate* na mabaki ya wanyama wa bahari ya kale. Hii ndiyo sababu visukuku vingi vinapatikana kwenye chokaa.

Aztec Sandstone

Aztec Sandstone inapatikana kwenye sehemu ya kusini/magharibi. Aztec Sandstone inajulikana kuwa *Navajo Sandstone* vile vile. Aina ya mawe ya mchanga hii ndiyo ngumu sana. Jabali kwenye Red Rock Canyon (red mountains) ni ya Aztec au Navajo Sandstone.

Concretions

Concretions ndiyo baadhi ya chuma (*iron oxide)* ambayo imewekwa kwenye mawe ya mchanga. Mawe yenye chuma hiyo yanatokea kama nguzo au tufe na kuonekana kuwa alama au nukta nyekundu au kuonekana kuwa mawe mviringo ya rangi ya kahawia juu ya mawe makubwa.

Visukuku

Visukuku ya matumbawe, wanyama mbalimbali ya chini ya Bahari, aina ya vijidudu yanayoitwa *bacteria* ya rangi ya blu na kijani, na vingine vinapatikana pale Red Rock Canyon. Nyayo za dinosau, mamalia, na wadudu zimepatikana kwenye mawe wa mchanga. Miti iliyofanya kuwa mawe (petrified wood) yanaonekana pia.

Tafadhali: Musiguse wala kuondoa visukuku ama mambo mengine ya zamani. Walakini, kupigia picha kunaruhusiwa.

Graffiti (Michoro)

Michoro ya mikwaruzo au maneno ya utuani hairuhusiwi po pote. Mtu anayefanya *graffiti* ataadhibiwa kwa kutozwa faini kubwa na kuwekwa gerezani. **Tafadhali:** Musichore, kukata wala kuchimbua mawe, vibao wala miti.